TAARIFA YA UTENDAJI NA UWAJIBIKAJI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

1.0 Utangulizi

Mhe. Mwenyekiti,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilianzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 ya mwaka 1982.

Mhe. Mwenyekiti,

Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji sura ya 288 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 pamoja na Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Tangazo la Serikali Na. 186 la mwaka 2015 kanuni ya 7(3)(c).

Mhe. Mwenyekiti,

Taarifa hii inaeleza shughuli zilizotekelezwa kwa idara na vitengo vya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

2.0 Utawala

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina jumla ya Kata kumi na sita **(16)** na Mitaa sabini na tatu **(73)**, ina jumla ya Madiwani **22,** kati ya hao Madiwani **16** wanaotoka katika Kata **16** zinazounda Halmashauri hii, na Madiwani sita **(6**) ni viti maalumu na Mbunge **1** wa Jimbo la Musoma mjini.

2.1 Utumishi

Halmashauri ina Idara **13** na vitengo **6**. Idara zenye wakuu wa Idara wenye Uteuzi rasmi ni kumi na moja **(11)** na Wakuu wa vitengo wenye uteuzi rasmi ni watatu **(3)**

2.2 Ikama ya watumishi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 - 2016/2017.

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mujibu wa ikama iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha **2015/2016 – 2016/2017** ina watumishi wapatao **1,731** ambapo mahitaji halisi ni watumishi **2,064,** hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **248.** Aidha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tumekasimia nafasi mpya **421** kwa kada mbalimbali.

Shughuli zilizotekelezwa na idara ni pamoja na kusimamia;

2.3 Utawala bora

Vikao vya kisheria ngazi ya Halmashauri

Kamati za Kudumu/Baraza	Lengo	Vikao vilivyofanyika	Asilimia ya vikao
	40	40	100

Vikao vya kisheria ngazi ya Kata (WDC)

Idadi ya kata	Lengo	Vikao vilivyofanyika	Asilimia ya vikao
16	64	61	95

Vikao vya kisheria ngazi ya Mitaa

Idadi ya Mitaa	Lengo	Vikao vilivyofanyika	Asilimia ya vikao
73	584	292	60

2.4 Mashauri ya Nidhamu

Katika mwaka wa Fedha 2016/2017, Halmashauri imeendesha Mashauri ya Nidhamu **15** kwa watumishi wake na watumishi watatu wanakesi mahakamani **3** hadi kufikia Juni 30, 2017 Mashauri hayo yalikuwa yamefikia hatua mbalimbali kama yanavyosomeka kwenye jewdwali hapo chini.

Watumishi waliopewa adhabu ya Onyo	Kuvuliwa Madaraka	Kushushwa Cheo	Kufukuzwa Kazi	Walioandikiwa hati za mashitaka	Wenye kesi Mahakamani	Jumla
8	1	1	4	1	3	18

2.5 Watumishi waliostaafu kwa mwaka wa fedha 2016/2017

Ke	Me	Jumla
22	16	38

2.6 Uhakiki wa Watumishi na Zoezi la Vitambulisho vya Taifa

Zoezi la Uhakiki wa Watunishi na Usajili wa Vitambulisho vya Taifa kwa watumishi wa Umma lilikamilishwa tarehe 15/07/2017. Zoezi hili lilitokana na maagizo ya Serikali kupitia Katibu Mkuu Utumishi kwa barua ya tarehe **21/09/2016** yenye **Kumb Na. CFC 26/295/01/56** iliyoelekeza kufanya uhakiki na utambuzi wa watumishi wa umma kwa kuunganisha utambuzi wa watu na mifumo mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali watu na mishahara katika utumishi wa umaa.

Hatua hii ililenga kuwezesha mifumo ya kielekroniki ya **usimamizi wa rasilimali watu na mishahara kutumia kanzi data (database)** ya utambulisho wa Taifa ya **NIDA,** ili kupata taarifa zao sahihi zikiwemo za kibaolojia; alama za vidole na cheki namba katika kutambua watumishi wa umma na mambo muhimu yanayohusiana na utumishi wao. Zoezi hili lilihusisha watumishi **1,731** wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ambapo walipatiwa vitambulisho vya Taifa.

2.7 Uhakiki wa vyeti vya watumishi

Baraza la Mitihani la Tanzania liliendesha zoezi la uhakiki wa vyeti vya watumishi. Katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma zoezi hili lilifanyika kuanzia tarehe **24/10/2016** na lilikamilika tarehe **01/11/2016**. Watumishi wote walitakiwa kushiriki na Matokeo ya uhakiki huo yalikuwa kama yanavyosomeka kwenye jedwali hapo chini.

Matokeo ya uhakiki huo yalikuwa kama ifuatavyo.

Watumishi waliogushi	Watumishi wevye vyeti vyenye utata	Watumishi ambao hawakukamilisha (incomplete)
35	16	22

2.8 Taarifa za watumishi waliokata rufaa zoezi la uhakiki wa vyeti

Mtumishi mmoja kati ya 35 waliobainika kuwa na vyeti feki alikata rufaa na kuwasilisha vyeti vyake halisi Baraza la mitihani kwa uhakiki upya. Watumishi **16** waliokuwa na vyeti vyenye utata walielekezwa kuwasilisha vyeti vyao halisi Baraza la mitihani ili kushughulikia utata uliojitokeza. Aidha watumishi wote 51 waliogushi na wenye vyeti vyenye utata waliondolewa kwenye orodha ‘payroll’ ya malipo ya mishahara ya Serikali tangu tarehe **08/05/2017.**

2.8.1 Matokeo ya Rufaa

Baada ya kukata rufaa, Watumishi **13** kati ya **16** waliokuwa na vyeti vyenye utata na **(1)** mmoja aliekata rufaa kutokana na sifa ya kughushi vyeti wamebainika kuwa na vyeti halali na wamerejeshwa kwenye 'payroll' ya malipo ya mishahara ya Serikali tangu tarehe **06/07/2017**, watumishi **3** wameshindwa kuthibitisha uhalali wa vyeti vyao. Watumishi **21** wenye Incomplete tunaendelea kusubiria taarifa zao kutoka Ofisi ya Rais Utumishi.

2.9 Uhakiki wa watumishi wa umma kwa kutumia taarifa za kitambulisho cha taifa (NIDA) pamoja na taarifa watumishi katika mfumo wa HCMIS.

Tarehe **06/06/2017**, Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora aliagiza kufanyika zoezi la uhakiki wa watumishi wa umma kwa kutumia taarifa za kitambulisho cha taifa **(NIDA)** pamoja na taarifa za kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na Mishahara (**HCMIS-LAWSON).** Zoezi hili lilianza tarehe **12 Juni 2017** na kumalizika tarehe **15 Julai 2017.**

Shughuli zote zilizoainishwa hapo juu ziligharimu shilingi **700,944,774.95.**

3.0 Fedha na Biashara

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na kuweza kufikia asilimia 103.65 ya makisio kama jedwali lifuatalo linavyoonesha.

NA	AINA YA CHANZO	MAKISIO YA MWAKA	MAPATO JULAI - JUNI	%
1	Leseni ya biashara	213,530,000.00	229,682,029.77	107.56
2	Leseni ya vileo	11,640,000.00	12,586,169.39	108.13
3	Ushuru wa machinjio	46,980,000.00	50,620,000.00	107.75
4	Ushuru wa masoko	22,248,000.00	19,556,888.00	87.90
5	Ushuru wa samaki na dagaa	60,000,000.00	117,233,198.00	195.39
6	Ushuru wa maegesho	39,576,000.00	35,716,150.00	90.25
7	Mapato mengineyo	-	44,738,947.02	-
8	Ushuru wa huduma	299,101,000.00	252,302,819.21	84.35
9	Leseni za mitumbwi	15,263,000.00	22,984,000.00	150.59
10	Ushuru wa matangazo	116,124,000.00	157,758,577.28	135.85
11	Kodi ya vibanda	267,181,000.00	206,917,655.60	77.44
12	CHF/ User fee	144,000,000.00	86,237,279.00	59.89
13	Ada ya kunyonya maji taka	27,360,000.00	6,314,159.00	23.08
14	Kodi ya ardhi	80,989,000.00	22,533,626.37	27.82
15	Adhabu ya ukiukaji wa sheria	6,120,000.00	5,113,500.00	83.55
16	Maombi ya zabuni	23,500,000.00	22,141,000.00	94.22
17	Ushuru wa stendi za magari	119,718,000.00	123,149,500.00	102.87
18	Usajili wa magari ya biashara	8,521,000.00	3,422,000.00	40.16
19	Ushuru wa maeneo ya kuoshea magari	8,640,000.00	1,110,000.00	12.85
20	Ushuru wa samaki toka viwandani	-	3,600,000.00	-
21	Ushuru wa nyumba za wageni (hotel levy)	102,282,000.00	39,549,439.00	38.67
22	Kodi ya pango ya minara ya simu	22,000,000.00	29,309,472.00	133.22
23	Ada za shule	-	178,967,000.00	-
24	Kodi ya majengo	-	22,964,956.68	-
	Jumla	**1,634,773,000.00**	**1,694,508,366.32**	**103.65**

ii. Kuandaa taarifa za mapato na matumizi kila mwezi na kila robo mwaka.

iii. Kuandaa na kuratibu malipo kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za fedha za Serikali za Mitaa.

iv. Kusimamia ufungaji wa hesabu za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa wakati na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo zilipelekea Halmashauri kupata **Hati safi** kwa hesabu za mwaka wa fedha 2015/2016.

v. Kujibu hoja za ukaguzi za mwaka wa fedha 2015/2016 kwa wakati na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

vi. Kutoa leseni za biashara kwa wafanyabiashara **3,011**

vii. Kutoa leseni za vileo kwa wafanyabiashara **321**.

viii. Kusimamia masoko **6** ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ambayo hutumiwa na wafanyabiashara wadogo wadogo kutoa huduma mbalimbali za biashara za nafaka, mbogamboga, matunda, samaki, nyama na bidhaa za madukani.

ix. Kufuatilia uzalishaji katika viwanda vikubwa. Manispaa ya Musoma inavyo jumla ya viwanda **8** vya uzalishaji bidhaa mbalimbali ambazo ni maziwa, samaki, maji, nguo na uchambuzi wa pamba **(Ginnery).** Hadi mwishoni mwa kipindi cha mwaka 2016/2017 viwanda **2** tu ndio vilikuwa vinazalisha bidhaa;

- Musoma Processing - Samaki
- ASTICA Group - Maji.

Viwanda **6** vimeshindwa kuzalisha bidhaa kwa sababu mbalimbali kama vile ukosefu wa malighafi, mtaji, uchakavu wa mitambo na gharama kubwa za uendeshaji.

x. Idara kwa kushirikiana na Taasisi, Makampuni na Mashirka mbalimbali walitoa mafunzo mbalimbali yanayowalenga wafanyabiashara mbalimbali **463** kama vile:-

a) Uendeshaji wa Biashara ya mafuta ya nishati (EWURA).
b) Usajili wa majina ya Biashara Makampuni, Alama za biashara na Hataza **(BRELA).**
c) Elimu ya Mlipa kodi **(TRA).**
d) Umuhimu wa wafanyabiashara wadogo (Wamachinga) kutumia masoko na maeneo rasmi ya biashara **(OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA).**
e) Elimu kwa wamiliki na waendesha Pikipiki za biashara (Bodaboda) **(POLISI, SUMATRA, NSSF, NHIF).**

Aidha, Wafanyabiashara wa kati na wadogo walishiriki maonesho mbalimbali ya biashara.

- Sabasaba - Dar Es Salaam.

- Nanenane - Mwanza.
- SIDO - Mwanza

Shughuli zote zilizoharimu shilingi **48,868,597.65.**

4.0 Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji

Idara ilitekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kuratibu na kuandaa Mpango na bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2017/2018.
ii. Kuandaa mpango kazi (Action plan) wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2016/2017
iii. Kushiriki katika kuandaa wasifu wa Mkoa wa Mara na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
iv. Kuandaa taarifa mbalimbali kama vile za miradi ya maendeleo kila robo mwaka kwa mwaka wa fedha 2016/2017, taarifa za utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2015.
v. Kuratibu majibu ya utekelezaji wa maagizo ya viongozi mbalimbali.
vi. Kuanza maandalizi ya Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
vii. Kutoa mafunzo juu ya Utaratibu ulioboreshwa wa Uendeshaji wa Ruzuku ya Maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGDG) kwa wajumbe wa Kamati za Maendeleo ya Kata (WDC).
viii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Shughuli zote zilizoharimu shilingi **78,038,500.00.**

5.0 Mipango miji na Ardhi

Idara ya Mipango Miji katika kipindi hiki imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka **1999**, Sheria ya Mipango Miji Na. **8** ya mwaka **2007**, Sheria ndogo za Halmashauri, miongozo na maagizo mbalimbali yaliyotolewa katika nyakati tofauti kutoka kwa viongozi mbalimbali.

Zifuatazo ndizo kazi zilizotekelezwa na Idara kwa mwaka wa fedha 2016/2017:-

i. **Kukamilisha kuandaa Mpango Kabambe (Musoma Master Plan 2015-2035).**

Idara ilikuwa na wajibu wa kufuatilia ukamilishaji na uidhinishwaji wa Master Plan ya Musoma. Jukumu hili limekamilika na Master Plan hiyo ilisainiwa rasmi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Mhe.William Lukuvi** tarehe **27/04/2017.**

ii. **Kuandaa michoro ya mipango miji.**

Idara ilikuwa imepanga kuandaa michoro **12** ya mipango miji katika maeneo ya Nyabisare, Mkendo eneo la ofisi za Serikali, Songe maeneo ya urasimishaji, Nyakato eneo la ofisi ya CCM na Kituo cha Afya, Buhare na sehemu ya Kigera. Hadi kufikia tarehe 30/6/2017 jumla ya michoro **16** ilikuwa imeandaliwa. Ongezeko hili limetokana na michoro ya zoezi la urasimishaji.

iii. **Uandaaji wa Hati miliki**.

Idara ilikuwa na lengo la kuandaa hati miliki **500** na hadi tarehe 30 Juni 2017 jumla ya Hati **461** zilimetayarishwa katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri kulingana na wananchi walivyokuwa wanajitokeza kuomba kuandaliwa hati. Aidha hati hizo ziliwasilisha kwa Msajili wa Hati Kanda ya Ziwa Mwanza kwa ajili ya kusajiliwa.

iv. **Ukusanyaji wa Pango la kodi ya Ardhi na Ada zingine zitokanazo na Ardhi**.

Idara ilipewa lengo la kukusanya jumla ya shilingi **500,000,000.00** ikiwa ni kodi ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2017 jumla ya shilingi **654,771,108.34** zimekusanywa ikiwa ni kodi ya Ardhi na kuvuka lengo kufikia asilimia **130.95%.**

v. **Utatuzi wa migogoro ya ardhi**.

Idara kwa kipindi hicho ilijikita kutatua migogoro yote ya ardhi inayoletwa kila siku na pia kumaliza migogoro ya nyuma kwa lengo la kuwapunguzia wananchi usumbufu unaotokana na migogoro hiyo. Aidha katika kipindi hicho Mkuu wa Wilaya ya Musoma kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma aliunda Tume ya kutatua migogoro ya ardhi ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza kero za wananchi zilizotokana na migogoro ya ardhi. Jumla ya malalamiko **162** yalipitiwa na kwa ujumla wake migogoro iligawanywa katika makundi yafuatayo;-

migogoro/malalamiko ya fidia yalikuwa **126**, malalamiko ya kiwanja kimoja kuwa na zaidi ya mtu mmoja (double allocation) ilikuwa **15** na migogoro iliyotokana na maamuzi ya mahakama ilikuwa **21**.

vi. **Upimaji wa maeneo ya umma**.
Idara ilikuwa na jukumu la kupima maeneo 6 ya umma ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ikijumuisha shule za sekondari 2 (Kamunyonge na Nyamiongo), shule za msingi 2 (Nyarigamba na Mshikamano) pamoja na maeneo ya huduma za afya 2 (Makoko na Buhare). Kazi hii haikukamilika kutokana na kukosa Mpima Ardhi.

vii. Kusimamia zoezi la uthamini wa mali za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

viii. Kuandaa ilani 2,053.

ix. Kuandaa michoro 6 ya mipango miji.

vii. Kuhamasisha na kupanda jumla ya miche **49,646** katika maeneo yafuatayo Barabara ya Majita kuanzia kituo cha polisi na Old custom , taasisi za serikali na maeneo ya watu, binafsi.

viii. Shule mbalimbali zikiwemo za Kiara sekondari, Nyasho sekondari,na Musoma ufundi zimetembelewa na kuzihamasisha kupanda miche ya miti.

ix. Doria 55 zimefanyika kwenye mlima Mukendo kudhibiti ukataji wa miti.

x. Utunzaji wa miche ya miti katika busitani ya miche ya Mkendo(EPC) umefanyika na mpaka sasa kuna jumla ya miche ya miti 3620 ina endelea kutunzwa.

xi. Utunzaji wa busitani ya kupumzika ya Mukendo(EPC) imefanyika.

Shughuli zote ziligharimu shilingi **106,213,463.90** kuzitekeleza.

6.0 Kitengo cha Teknolojia, Habari, Mawasiliano na uhusiano

Shughuli zilizotekelezwa na Kitengo cha Teknolojia, Mawasiliano, Habari na Uhusiano katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017;

i. Kuratibu na kusimamia waandishi wa Habari katika matukio kumi na sita (16) ya Halmashauri kama Baraza la Madiwani(Full Council), Utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara za mjini na matukio mengine yanayohitaji kuhabarishwa kwa umma kupitia vyombo vya Habari.

ii. Uchukuaji na uhifadhi wa matukio muhimu yaliyofanyika katika Manispaa ikiwa ni uchukuaji wa picha za mnato, video na sauti. Jumla ya picha za

mnato **465**, video **20** pamoja na uchukuaji wa sauti (audio recording) 'Clips' **34** umefanyika.

iii. Kitengo kimekamilisha utengenezaji wa tovuti ya Halmashauri. Uingizaji na uhuishaji wa taarifa katika tovuti hufanyika mara kwa mara. Tovuti inapatikana kwa anwani ya ***www.musomamc.go.tz*.**

iv. Uandishi wa makala, Uhariri wa picha za mnato na video, Ukusanyaji wa taarifa muhimu za idara mbalimbali kwa ajili ya kuziingiza kwenye tovuti ya Halmashauri umefanyika. Jumla ya makala **25**, Habari **21** zimeandikwa na kuwekwa katika tovuti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

v. Uratibu wa malalamiko ya wananchi umefanyika. Jumla ya malalamiko **41** yalipokelewa na kupelekwa idara husika kwa ajili ya utatuzi ambapo kati ya malalamiko **41** yaliyopokelewa **33** yamekamilika na **8** yako katika hatua mbalimbali za utatuzi.

vi. Utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA katika idara mbalimbali ili kuhakikisha usalama na utendaji kazi wake unakuwa katika hali nzuri.

vii. Kitengo kimehakikisha mifumo ya TASAF, EPICOR, HCMIS, BEMIS na LGRCIS inakuwa katika usalama pamoja na kuendelea kufanya kazi ipasavyo.

viii. Mradi wa "**Government Communication Network''** (GoveNet) Umeanza kutekelezwa katika Halmashauri yetu. Uwekaji wa Mtandao Kiwambo (**Local Area Network**) umekamilika kwa asilimia **99**. Mkandarasi kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri yetu wameshawasha baadhi ya mitambo. Hadi sasa ofisi zote za wakuu wa idara na vitengo zimeunganishwa kwa mawasiliano ya simu za kisasa yaani IP-PHONES, ikiwa ni sambamba na upatikanaji wa huduma ya internet. Kukamilika kwa mradi huu pamoja na mambo mengine kutaiwezesha Halmashauri yetu kupata mawasiliano ya haraka, salama, teknolojia ya kisasa na madhubuti. Aidha tutaweza kupiga simu (audio &video) katika taasisi nyingine za serikali zilizounganishwa bila gharama za ziada.

Shughuli zote zilizogharimu shilingi **8,345,000.00.**

7.0 Mifugo na Uvuvi

Shughuli zilizopangwa na kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 ni;

i. Kuanza ukarabati wa machinjio kuu ya Bweri ambapo utekelezaji uko kwenye hatua ya awali.
ii. Ununuzi wa chanjo za kichaa cha mbwa vichupa **100** (dozi 1,000) ambapo utekelezaji upo katika hatua ya manunuzi.
iii. Zoezi la utambuzi, uandikishaji, usajili, upigaji wa chapa na uwekaji kumbukumbu za mifugo kwa ngombe **4,700**, mbuzi na kondoo **4,510** ambapo utekelezaji unaendelea kwa kutoa elimu juu ya umuhimu wa zoezi japo fedha zilizotengwa hazikutolewa.
iv. Kuimarisha ukaguzi wa afya za mifugo na mazao yake na ukusanyaji wa ushuru wa machinjio ambapo jumla ya mifugo **14,641** ilikaguliwa na nyama kuruhusiwa kwa matumizi ya binadamu.
v. Kufanya utambuzi wa magonjwa ya mifugo,ufuatiliaji na utoaji wa kinga na tiba kwa mifugo **16,674**.
vi. Kuingiza taarifa za mifugo na uvuvi kwenye mfumo wa ARDS za kila mwezi taarifa **12**, robo taarifa **4** na taarifa ya mwaka.
vii. Uhamilishaji wa mifugo kwa kutumia mbegu za madume bora kwa kupandisha ngombe wa kisasa **252** na ngombe wa asili **1,521** utekelezaji uliofanyika ni kutoa elimu husika japo fedha tengwa hazikutolewa.
viii. Kusimamia na kufuatilia uboreshaji wa zao la ngozi kwa kufanya ukaguzi wa mabanda 4 ya ngozi, utoaji wa vibali vya kusafirisha ngozi na bidhaa zake.
ix. Kutoa elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji **1,154**.
x. Kufanya doria **21** ndani na nje ya Ziwa Victoria pamoja na kutoa elimu juu ya uvuvi endelevu kwa wadau **191** walioko kwenye mialo.
xi. Kutoa leseni za mitumbwi **27** na ukusanyaji wa mapato yatokayanayo na vyanzo vya Uvuvi.
xii. Kutoa elimu juu ya ufugaji bora wa samaki kwa wadau **47.**

Shughuli zote ziligharimu jumla ya shilingi **18,225,000.00.**

8.0 Usafishaji na Mazingira

Idara ya Usafishaji na Mazingira inaendelea kusimamia huduma za Afya ili kupambana na magonjwa ya kuambukiza na ya milipuko katika jamii na kulinda mazingira. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa;

i. Kutoa huduma ya usafi wa mazingira kwa kufagia barabara zipatazo **297**, masoko **6** na stendi **3**.
ii. Kusafisha na kuzibua mifereji ya maji ya mvua ipatayo **198**.
iii. Kukusanya, kusomba na kutupa taka ngumu kutoka kwenye Kaya na vizimba zenye uzito wa tani **20,866**.
iv. Kufyeka nyasi maeneo ya wazi mita za mraba **52** kando kando ya barabara na sehemu za wazi kudhibiti mbu, wadudu na wanyama hatari.
v. Kufanya ukaguzi wa majengo mbalimbali **17,148** zikiwemo nyumba za kuishi, majengo ya biashara, Taasisi binafsi na za Umma na kutoa elimu ya Afya kuzingatia usafi wa mazingira.
vi. Kutoa huduma ya mazishi kwa marehemu **29** wasiokuwa na ndugu.
vii. Kufanya kaguzi katika Mitaa **73** kutambua kuwepo kwa mazalio ya mbu **680** na kuchukua hatua.
viii. Kukagua na kusimamia usajili wa majengo **462** kuthibiti ubora wa chakula, dawa na vipodozi.
ix. Kufuatilia mwenendo wa magonjwa na kutuma taarifa **48** za kuwepo au kutokuwepo kwa magonjwa hatari **12** ya milipuko.
x. Kuagiza na kusambaza chupa za chanjo **32,700** katika Zahanati na vituo vya Afya.
xi. Kuhimiza kaya **758** kuchimba, kujenga na kutumia vyoo bora na vibuyu chirizi.
xii. Kutoa mafunzo ya Elimu ya Afya katika mitaa **73** juu ya utupaji wa taka ngumu, taka maji na utumiaji wa vyoo bora ngazi ya kaya.
xiii. Kukusanya takwimu kutoka kaya **3,20**8 kutathimini matumizi ya vyoo bora.
xiv. Kuratibu zoezi la usafi wa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.
xv. Kufanya usimamizi elekezi kusimamia utendaji wa watumishi katika kata.

Aidha katika kutekeleza shughuli za mazingira idara ilitekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kuzijengea uwezo Kamati za Mazingira za mitaa, kata na ngazi ya Manispaa. Semina elekezi ilitolewa kwa kamati za mazingira za mitaa **73**,

kata zote **16** pamoja na Waheshimiwa madiwani wote. Mada kuu ilikuwa ni kuzijengea uwezo kamati za mazingira ngazi zote katika kutambua majukumu yao ili kuleta ufanisi wa kamati za mazingira katika usimamizi wa mazingira.

ii. Kusimamia kufanyika kwa maadhimisho ya siku ya mazingira Afrika tarehe **3 Machi, 2017** na Siku ya mazingira Duniani tarehe **1-5 Juni, 2017**. Wakati wa maadhimisho haya jumla ya **miti 11,251** ilipandwa katika maeneo mbalimbali hususan mashuleni na kwenye hifadhi za barabara.

iii. Jumla ya viwanda vikubwa **3** ambavyo ni Mutex, Musoma Fish Processors Limited na Serengeti water), viwanda vidogo **5**, mradi wa kukoboa mpunga wa Mudeko, vituo **10** vya kuuza mafuta (petrol stations), gareji **7,** vituo **12** vya kuoshea magari (car wash), shule **5** za msingi na sekondari na vituo **3** vya kuchenjua dhahabu vilitembelewa kwa ukaguzi na ufuatiliaji wa utunzaji mazingira.

iv. Wafanyabiashara wauza samaki **13** katika mwalo wa Mwigobero walipewa elimu kuhusu usafi wa Mazingira katika biahara zao za kuuza samaki.

v. Usimamizi wa mchakato wa tathmini ya athari kwa mazingira (**EIA na EA**) ulifanyika kuhusu miradi ya barabara za mjini na soko la Nyasho ambapo Halmashauri ilifanikiwa kupata vyeti vya EIA kwa miradi yote miwili mnamo mwezi machi, 2017 kutoka NEMC. Miradi mingine iliyosimamiwa ni Environmental Audit (EA) ya GAPCO Filling Stations, Afrioil pamoja na mradi wa miundombinu ya kukusanya na kutibu maji taka (sewerage system and waste water treatment plant) chini ya MUWASA.

vi. Kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazohusu usimamizi wa mazingira na shughuli maalumu za kisekta zinazohusiana na mazingira.

vii. Kitengo cha mazingira kilishiriki katika utungaji wa sheria ndogo za usimamizi wa mazingira za mwaka 2016 pamoja na sheria ndogo zingine kama sheria ndogo za kudhibiti madini ujenzi.

viii. Mchakato wa Kuutangaza mlima Mukendo kuwa eneo la mazingira lindwa ulifanyika kutokana na msitu wa asili uliopo pamoja na wanyama na ndege waliomo kwenye mlima huo ili kupunguza uharibifu wa mazingira na kuhifadhi msitu huo na viumbe waliomo. Pendekezo hili lilipitishwa katika ngazi zote za halmashauri na kupelekwa NEMC. Timu ya NEMC ilishakwisha tembelea mlima kwa hatua zaidi.

ix. Taarifa za robo zote (robo ya I-IV za mwa 2016/2017) ziliandaliwa. Taarifa za robo hutoa ufafanuzi kuhusu masuala ya mazingira na usimamizi wake ulivyofanyika katika kipindi cha robo husika.

Shughuli zote za idara ziligharimu shilingi **91,120,000.00.**

9.0 Afya

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kufanya ukaguzi wa maduka ya dawa muhimu **101** na maabara **26** za watu binafsi.
ii. Kufanya ukaguzi wa matumizi ya dawa (drug audit) katika vituo vya kutolea huduma za afya.
iii. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya afya **2** na zahanati 8 ambapo dawa na vifaa tiba viliweza kununuliwa kutoka Bohari kuu ya dawa MSD.
iv. Kufanya matengenezo ya vifaa tiba vilivyo haribika katika vituo vya afya **2** na zahanati **8**.
v. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya afya **2** na zahanati **8**.
vi. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya afya 2 na zahanati **8**.
vii. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya wagonjwa katika vituo vya afya **2** na zahanati **8**.
viii. Kutengeneza mabakala (shelves) ya kutunzia dawa katika stoo ya dawa ya kituo cha afya Nyasho na hivyo utunzaji wa dawa na mafaili ya wagonjwa umeboreshwa.
ix. Kununua mafuta maalumu kwa ajili ya walemavu wa ngozi (albino) ili kuwakinga na magonjwa ya ngozi ambapo chupa za mafuta **116** zilinunuliwa na wagonjwa wa ngozi (albino) **33** waliweza kupatiwa mafuta hayo na yaliyobaki yalipelekwa katika shule ya msingi Mwisenge “B”.
x. Kununua vifaa vya ofisi kwa ajili ya kuwapiga picha wazee na kuwatengenezea vitambulisho vya matibabu ambapo vifaa vimenunuliwa na wazee **1,702** walioko katika kata **9** wamepigwa picha na wazee **212** wamepatiwa vitambulisho vya matibabu na zoezi linaendelea.

xi. Kuwawezesha watoa huduma **73** ngazi ya jamii kusajili mama wajawazito **458** na watoto na watoto **4,828** chini ya miaka mitano katika jamii.

xii. Kufanya vikao vya kujadili vifo vya wajawazito na watoto wachanga ili kujua sababu za vifo hivyo na kuweka mikakati ya kudhibiti vifo hivyo.

xiii. Kuchapisha kadi za kliniki (RCH) **3,000** kwa ajili ya matumizi ya vituo vya afya na zahanati katika kufuatilia ukuaji wa watoto.

xiv. Kukusanya chupa za damu salama **625** ambapo wagonjwa **168** wenye uhitaji wa damu walipatiwa damu salama katika kituo cha afya Nyasho na hivyo kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

xv. Kufanya mafunzo ya siku tano kwa watumishi **22** wa afya kuhusu uchunguzi wa kansa ya shingo ya kizazi kwa wanawake.

xvi. Kujaza Mitungi ya gesi **84** kwa ajili ya utunzaji wa chanjo katika vituo vya afya na zahanati.

xvii. Kuwawezesha watumishi wa afya kufanya kampeni ya utoaji matone ya vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto chini ya miaka mitano mara mbili kwa mwaka ambapo jumla ya watoto **46,032** chini ya miaka mitano walipewa huduma hiyo.

xviii. Kununua matairi na kufanya matengenezo ya magari ya idara ya afya kwa ajili ya kuwezesha rufaa za wagonjwa na shughuli za usimimazi na chanjo ambapo magari **3** (ambulance 2 na gari la chanjo) yalinunuliwa matairi na magari Na. DFPA 2909, SM 4088, SM 4666, DFP 4385 na STK 7106 yalifanyiwa ukaguzi na kutengenezwa ili kuimarisha rufaa za wagonjwa na shughuli zingine za afya.

xix. Kununua mafuta kwa ajili ya magari ya idara ya afya na jenereta ili kuwezesha rufaa za wagonjwa, shughuli za usimimazi, chanjo na huduma za upasuaji.

xx. Kupima maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa wateja **1,051** (wanaume 303 na wanawake 748) katika siku ya maadhimisho ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 kati ya hao watu **9** (1%) walikutwa na maambukizo.

xxi. Kuwawezesha watumishi wa afya 4 wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kupata lishe ili kuboresha afya zao na kuwakinga na magonjwa nyemelezi.

xxii. Kununua vyandarua **33** vyenye viuatilifu kwa ajili ya kuwapatia wagonjwa.

xxiii. Kununua mashine ya kufulia nguo za wagonjwa katika kituo cha Afya Bweri.

xxiv. Kujenga sehemu za kufulia nguo za wagonjwa (washing slabs) kwa ajili ya vituo vya Afya Nyasho na Bweri.

xxv. Kusimika matenki ya maji matatu (3) katika zahanati za Buhare, Nyakato na Nyamatare kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji.

xxvi. Kununua samani (makabati, benchi, viti na meza) za ofisi kwa ajili ya zahanati ya Nyamatare.

xxvii. Kufanya kikao cha siku mbili cha watumishi wa afya , ustawi wa jamii na maafisa wa polisi jinsi ya kuwahudumia waanga wa ukatili wa kijinsia.

xxviii. Kutoa zawadi ya wafanyakazi hodari 3 wa idara ya afya siku ya Mei Mosi kwa mwaka 2017.

xxix. Kulipa stahiki mbalimbali za watumishi za watumishi wa afya **184** ambapo jumla ya watumishi **108** waliweza kulipwa stahiki zao kama likizo, fedha za matibabu, masaa ya ziada, fedha za mazishi, sare za kazi na fedha za kusafrisha mizigo kwa wastaafu.

xxx. Kuwalipia ada watumishi **2** wanaosoma katika vyuo.

xxxi. Kuwezesha ofisi ya Mganga Mkuu wa manispaa kufanya kazi ambapo shajara, malipo ya bili za maji, umeme na gharama nyingine za ofisi ziliweza kushughulikiwa.

xxxii. Kuitisha vikao **2** vya bodi ya afya.

xxxiii. Kuitisha kikao na watumishi cha ufuatiliaji na tathmini ya utoaji huduma katika vituo **27** vya kutolea huduma za Afya.

xxxiv. Kuwawezesha wajumbe 18 wa CHMT kufanya usimamizi elekezi/shirikishi safari 50 kwa mwaka katika vituo vya kutolea huduma za afya **27**.

xxxv. Kufanya uhamasishaji katika kamati za maendeleo za kata za Iringo, Mukendo, Kitaji na Mwigobero juu ya matumizi ya madini joto na lishe ili kupunguza magonjwa yatokanayo na lishe duni.

xxxvi. Kuandaa mpango kabambe wa Halmashauri wa Afya (CCHP) kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na Mipango **10** ya vituo vya afya **2** na zahanati **8** na kuiwasilisha OR-TAMISEMI kwa uhakiki.

xxxvii. Kufanya uhamasishaji wa jamii kujiunga na Mfuko wa afya wa Jamii (CHF) katika kamati za maendeleo za kata 7 (Makoko, Kamunyonge, Mshikamano, Bweri, Nyasho, Kigera na Kwangwa) na kaya **1,099 (14%)** zimejiunga katika Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) kwa mwaka 2016/2017.

xxxviii. Kuwafanyia uchunguzi wa magonjwa ya Kichocho na Minyoo ya tumbo wanafunzi **288** wa shule 2 za msingi za Musoma na Nyasho “A” na kati ya

hao wanafunzi **17** walikutwa na Minyoo ya tumbo, wanafunzi **3** walikutwa na Kichocho na wanafunzi **42** walikutwa na matatizo mengine mbalimbali na wote walitibiwa.

xxxix. Kukamilisha ujenzi ya wodi ya wazazi katika kituo cha afya Bweri na kazi inaendelea.

xl. Kukarabati vyumba kwa ajili ya huduma rafiki za afya kwa vijana katika vituo vya afya vya Nyasho, Bweri na Bethsaida na zahanati ya Kwangwa.

Jumla ya fedha kiasi cha shilingi **378,625,489.00** zilitumika.

10.0 Elimu msingi

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kukamilisha maandalizi ya mtihani wa Taifa wa darasa la IV, VII 2016.

ii. Kusajili watahiniwa **4,191**wa mtihani wa Taifa Darasa VII na upimaji wa Darasa IV – 2017.

iii. Kuratibu na kusimamia mtihani wa Taifa wa darasa VII – 2016.

- Waliosajiliwa ni **4,191** (Wav 1,986 na Was 2,205)
- Waliofanya mtihani ni **4,169** (Wav 1,973 na Was 2,196)
- Waliofaulu ni **3,445** (Wav 1,765 na Was 1,680)
- Asilimia ya ufaulu ni **82.63**.

iv. Kuratibu na kusimamia mtihani wa darasa IV 2016.

v. Kuandaa orodha kuu ya wanafunzi wa Kidato cha I – 2017.

vi. Kuratibu, kusimamia na kusahihisha mtihani wa majaribio wa Mkoa Darasa VII – 2017.

vii. Kufanya vikao, mikutano ya kiutendaji kwa Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu.

viii. Kufanya ufuatiliaji wa utendaji kazi kwa Walimu na wanafunzi kwa Shule 52.

ix. Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa wafanyakazi bora na zawadi zao.

x. Kuwapatiwa mafunzo Walimu **54** ya kufundisha KKK (3 Rs Inset).

xi. Kutoa mafunzo ya kuboresha shule (Inset General) kwa Walimu, MEK na Maafisa Elimu.

xii. Kutoa mafunzo ya kuziongezea Shule **38** kipato (School Income Generating activities).

xiii. Kuwapatia mafunzo Walimu na Waratibu Elimu Kata juu ya uongozi na utawala (School leadership and Management).

xiv. Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za “Capitaion” na kutoa taarifa kila zinapowekwa katika akaunti za shule.

xv. Kuendesha semina za ukusanyaji, uandaaji na utengenezaji wa takwimu za elimu shuleni na katani kwa MEK na walimu wakuu.

xvi. Kutembelea Shule **42** kukagua na kuhimiza ulinzi na utunzaji bora wa mali zote za shule (Miundombinu, Samani, Vitabu, n.k).

xvii. Kufuatilia upatikanaji wa chakula, maji, umeme na afya za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

xviii. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo ya elimu ya Msingi (MMEM) wa kila robo mwaka.

xix. Kujenga choo cha walimu na wanafuzni shule ya Msingi Mwisenge "A" chenye matundu **10** na na JTWZ Bukanga chenye matundu **10.**

xx. Kujenga na kukamilisha vyumba **13** vya madarasa na choo shule ya msingi za Mwisenge “B” (04), Kambarage “A” (02), Kigera “A” (02), Rwamlimi “B” (02), JWTZ Bukanga (02) na Kapt. Msangi (02).

xxi. Kukarabati ofisi ya walimu na Ofisi ya Mwalimu Mkuu shule ya msingi Mwisenge “B”

xxii. Kuanza ujenzi wa vyumba vya madarasa **14** katika shule za msingi za Bweri (02), Bukoba (02), Kambarage “A” (03), Kambarage “B” (02), Nyamatare “A” (01), Nyamatare “B” (01) na Mtakuja ‘B” (03). Hatua ya ujenzi iko hatua za msingi.

Jumla ya fedha kiasi cha shilingi **696,121,702.00** zilitumika kutekeleza kazi hizo.

11.0 Elimu Sekondari

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kusimamia uwajibikaji na utendaji kazi kwa walimu na watumishi wasio walimu na kufanya tathmini ya utendaji kazi kila mwezi.

ii. Kushiriki kuhakiki madai ya walimu kuanzia Januari, 2015 hadi Desemba, 2015.

iii. Kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa 8 (2 Nyamiongo sekondari, 2 Iringo Sekondari na 4 Nyasho Sekondari) yamejengwa, ukarabati wa vyumba vya madarasa madarasa **14** (Nyamiongo 6, Iringo 2 na Nyasho 6),

ujenzi wa matundu ya vyoo **56** (Nyasho Sekondari 10, Nyamiongo 18, Iringo 18 na Morembe Sekondari 10).

iv. Kuendelea na ukarabati mkubwa wa majengo katika shule ya Sekondari Musoma.

v. Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule za Sekondari (Capitation grant, Fidia ya Ada na Chakula cha wanafunzi).

vi. Kusimamia uendeshaji wa mitihani ya Kitaifa kwa kidato cha II, IV na VI ufaulu ulikuwa kama ifuatavyo;

- Kidato cha II, 2016 - **94%**
- Kidato cha IV, 2016 – **65%**
- Kidato cha VI, 2016 – **98.2%**

vii. Kusimamia shughuli za michezo katika shule za Sekondari ambapo wanafunzi walishiriki michezo ya UMISSETA kuanzia ngazi ya Shule, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.

viii. Kupokea na kusambaza vifaa vya kundishia na kujifunzia (vitabu kwa shule **18** na vifaa vya maabara kwa shule **5**) katika shule za Sekondari za Serikali. Jumla ya vitabu **13,530** vya masomo ya sayansi, Hisabati Lugha na Sanaa vilipokelewa na kusambazwa katika shule za Sekondari za Serikali na vifaa vya maabara vilipokelewa kwa ajili ya shule za sekondari za Kamunyonge, Mara, Morembe, Musoma na Nyamitwebiri.

ix. Kupanga walimu **14** wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

Jumla ya fedha kiasi cha shilingi **2,431,623,999.00** zilitumika kutekeleza kazi hizo.

12.0 Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kufanya vikao **10** vya idara kuwapatia watumishi uelewa wa pamoja kuhusu shughuli zitakazotekelezwa na idara.

ii. Kutoa mafunzo kwa wakulina kuhusu kilimo bora cha zao la nyanya ambapo wakulima **25** walipata mafunzo ya siku nne kuhusu kilimo bora cha zao la nyanya na magonjwa yanayoshambulia zao hilo. Pia wakulima **9** walipata mafunzo kuhusu uoteshaji na ubebeshaji wa miche bora ya matunda aina ya miparachichi, michungwa na miembe.

iii. Wataalamu wa ugani ngazi ya Halmashauri walifuatilia utendaji kazi wa wataalamu wa ugani ngazi ya kata mara kumi katika miezi kumi na mbili.

iv. Kuratibu hali ya chakula na upatikanaji wake ambapo takwimu za bei za vyakula zilichukuliwa kila wiki ili kupata wastani wa bei katika mwezi,

taarifa ya hali ya chakula kila Mwezi iliandaliwa na kutumwa Wilayani na Mkoani na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kila mwezi.

v. Kutoa huduma za ugani katika kata **16** za Manispaa ya Musoma kwa wataalamu wa ugani ngazi ya kata, kuwatembelea na kuwashauri wakulima ambapo wakulima **4,288** wa mazao ya mbalimbali katika Kata 16 za Manispaa ya Musoma walitembelewa na kupewa ushauri kuhusu kulima kwa kuzingatia kanuni bora za mazao wanayolima.

vi. Kukusanya takwimu za kilimo za kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka kutoka Kata **16** za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na kuziingiza katika mfumo wa Kompyuta wa "Agricultural Routine data System" (ARDS)- "Wep Portal".

vii. Kuhimiza na kuhamasisha maendeleo ya vyama vya ushirika 20 vilivyo hai ambapo jumla ya SACCOS **11** zilipata ushauri wa kisheria kupitia kikao cha pamoja kilichofanyika chini ya Mkuu wa Wilaya ambazo ni Musoma Municipal, Musoma Hospital, Musoma dairy, AIC Nyasho, Mara VETA, Mafanikio Mwigobero, Imara, Musoma Urban, Musoma, SHAMMAH na Umoja wa kahawa.

viii. Kuinua kiwango cha uelewa wa jamii ya vijana na vikundi vinginevyo kuhusu faida za asili za vyama vya ushirika katika kata 16 ambapo ushauri na elimu vilitolewa kwa viongozi wa vikundi 5 (Faraja-Bweri, Bora Tanzania-Mwisenge, Byangwe exploration and mining-Mkendo, Inuka-Nyakato na Maandazi- Nyasho).

ix. Kushiriki maonesho ya kilimo Nane nane 2016 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilipata ushindi wa nafasi ya 3 kati ya Halmashauri 36 zilizoshiriki.

x. Kuandaa taarifa za mwezi, robo mwaka na kuziwasilisha kwa wadau.

Shughuli zote ziligharimu shilingi **14,938,090,00.**

13.0 Maendeleo ya jamii

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuhamasisha uundaji wa vikundi vya uzalishaji mali kutoka katika kata 16 ambapo vikundi 146 vya uzalishaji mali viliundwa.

ii. Kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ya wanawake na vijana iliyotolewa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Juni, 2017. Ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ulifanyika na jumla ya shilingi **15,739,400.00** zimerejeshwa kutoka vikundi vya wanawake na shilingi **3,470,000.00** kutoka vikundi vya vijana.

iii. Kutoa mafunzo elekezi kwa vikundi vya wanawake na vijana vilivyopatiwa mikopo ambapo vikundi **75** vilipatiwa mafunzo elekezi baada kupatiwa

mikopo; **54** vya wanawake na **21** vya vijana.

iv. Kuhamasisha jamii kujiunga na mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Jumla ya kaya **1,099** zimejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii.

v. Kutambua asasi zisizokuwa za kiserikali ambapo asasi 4 zisizokuwa za kiserikali zilitambuliwa.

vi. Kufanya maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani na Siku ya Mtoto wa Afrika.

vii. Kusajili vikundi vya ujasiriamali **146** katika kata **16**.

viii. Kushughulikia kesi za ulinzi na usalama wa motto ambapo jumla ya kesi 162 zilishughulikiwa na kutafutiwa ufumbuzi.

ix. Kushughulikia mashauri **79** ya migogoro ya ndoa.

x. Kufanya utambuzi wa watoto wa mitaani, ambapo jumla ya watoto 18 walitambuliwa.

xi. Kufanya utambuzi wa watu wenye ulemavu ambapo jumla ya watu **261** wenye ulemavu wa akili, ngozi, viungo, viziwi na wasioona walitambuliwa katika kata zote **16**.

xii. Kufanya zoezi la upigaji picha kwa wazee kwa ajili ya kuwatengenezea vitambulisho vya matibabu, ambapo ni jumla ya wazee **1,702** walifikiwa, na **212** walipewa vitambulisho.

xiii. Kuendesha zoezi la uundaji wa kamati za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi (MVCC) katika kata mbili (2) za Nyakato na Mwisenge.

xiv. Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya na umuhimu wa upimaji wa VVU.

xv. Kufanya vikao na wadau na wanaoishi na VVU/UKIMWI ambapo kikao kimoja cha WAVIU na kimoja cha wadau.

xvi. Kutoa huduma ya upimaji wa VVU kwa hiari katika jamii ambapo upimaji wa VVU kwa watumishi wa mradi wa maji Bukanga ulifanyika.

xvii. Kutoa ruzuku kwa jkaya maskini **2,408** zilizopo kwenye mpango.

xviii. Kufanya usimamizi na ufuatiliaji ngazi ya Halmashauri, Mitaa na Kata wakati wa kutoa ruzuku kwa kaya maskini **2,408**.

Shughuli zote ziligharimu shilingi **618,226,589.00.**

14.0 Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi

Shughuli zilizotekelezwa na kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi kwa mwaka 2016/2017 ni kama ifuatavyo;

i. Kuratibu na kusimamia ununuzi katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ambapo Halmashauri ilitenga jumla ya shilingi **9,200,349,157.00** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ununuzi wa vifaa na bidhaa, huduma

zisizo za Kitaalam, Huduma za Ushauri wa Kitaalam na kazi mbalimbali za miradi. Hadi kufikia tarehe 30/06/2017 jumla ya shilingi **7,689,457,131.69** zilikuwa zimetumika katika shughuli za Ununuzi ambayo ni sawa na asilimia **83.6** ya ununuzi uliopangwa kwenye ngazi ya Halmashauri.

Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

Na	Aina ya Mahitaji yaliyopangwa 2016/2017	Kiasi cha fedha kilichotengwa 2016/2017	Fedha iliyotumika hadi 30/06/2017	Asilimia
1.	Kazi za Ujenzi (Works)	7,637,868,042.00	6,291,364,661.16	82.4%
2.	Vifaa na Bidhaa (Goods)	514,934,533.00	445,766,980.56	86.6%
3.	Huduma zisizo za Ushauri wa Kitaalam (Non – Consultancy Services)	149,546,582.00	58,847,089.97	39.35%
4.	Huduma za Ushauri ya Kitaalam	898,000,000.00	893,478,400.00	99.5%
	Jumla	**9,200,349,157.00**	**7,689,457,131.69**	**83.6%**

ii. Kuitisha vikao vya pmu na Bodi ya Zabuni ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2016/2017 Bodi ya Zabuni ilikaa vikao mbalimbali vya kawaida **13** na maamuzi kwa njia ya mzunguko (Circular Resolution) vikao **4** pamoja na vikao vya Kitengo cha Ununuzi na Ugavi ni **24** ikiwa ni kwa ajili ya ufunguzi wa zabuni mbalimbali na upitiaji wa taarifa mbalimbali za Ununuzi.

iii. Kuandaa Mpango wa Ununuzi wa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kuzingatia sheria ya ununuzi na 7 ya mwaka 2011, Kitengo kimeandaa Mpango wa Ununuzi wa Halmashauri utakaotumika katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za ununuzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wenye jumla ya shilingi **8,099,472,034.00.**

Shughuli zote zilizotekelezwa ziligharimu shilingi **12,924,500.00.**

15.0 Maji

Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama ifuatavyo;

i. Ukarabati wa miundombinu ya maji safi kwa ajili ya kuongeza wingi wa maji katika Soko kuu la Manispaa ya Musoma
ii. Kurudisha maji katika shule ya msingi Kapteni Msangi Nyakato

iii. Kufanya ukarabati wa mfumo wa maji safi na maji taka katika machinjio ya Bweri
iv. Uwekaji wa vigae soko kuu sehemu ya kuuzia samaki wabichi
v. Kuweka sahani za vyoo katika shule ya sekondari Iringo na Nyamiongo
vi. Kufanya ukarabati wa mfumo wa tanki la uvunaji wa maji ya mvua katika shule za msingi Bukoba, Kambarage Songambele na Rwamlimi na shule za sekongari Kamnyonge, Nyabisare na Morembe
vii. Kurudisha maji katika soko la nyasho
viii. Ukarbati wa mfumo wa maji safi na maji taka katika nyumba anamoishi Mkurugenzi na Afsa utumishi Manispaa ya Musoma
ix. Kufanya ukarabati wa pampu ya mkono katika shule ya walemavu Mwisenge
x. Kufanya ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji katika shule za sekondari za Songe na Musoma ufundi.

Shughuli zote zilitekelezwa kwa kutumia shilingi **15,838,625.00.**

16. Ujenzi

Idara ya ujenzi ilisimamia matengenezo ya barabara zilizotengenezwa kwa fedha zilizovuka mwaka wa fedha 2015/2016 na zile zilizoidhinishwa kwa mwaka 2016/2017. Matengenezo ya barabara yaliyosimamiwa kwa kutumia fedha zilizovuka mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama yafuatayo;

i. Matengenezo ya barabara za Magamaga, Anarlando,Nyakato, Nyabisarye, Nyakato Sa Nane, Nyakato Jumba la Dhahabu, Nyakato, Bweri maduka Tisa, Songambele. Mkandarasi alikuwa ni M/S KUMBA QUALITY CONSTRUCTION LTD, S.L.P. 261, TARIME.

ii. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Nyamatare & Kamunyonge Biafra, matengenezo ya sehemu korofi katika barabara za Nyamatare (Mzee Mtongori – SDA Church - Kamunyonge) na Matengenezo ya muda maalumu barabara za Haile Selasie, Peace Palace – Field Force, Kwangwa, Mara Sekondari – Kiara Buhare, Zahanati ya Kamunyonge SDA & Nyamatare. Mkandarasi alikuwa ni M/S WHITE DOOR (T) LTD, S.L.P. 1446, MUSOMA.

iii. Matengenezo ya kawaida barabara za makoko, buhare-mwisenge-makoko and buhare – kurumuli, matengenezo ya muda maalumu barabara za buhare, mtakuja-nyamiongo and mwisenge-majita pamoja na kalvati na mitaro barabara za buhare, mwisenge na mwisenge makaburini. Mkandarasi

alikuwa ni MAKIMA GENERAL TRADERS, S.L.P. 8356, DAR ES SALAAM.

iv. Ujenzi wa Daraja na Kalvati katika barabara za Kwangwa - kiara na Kiara – Buhare. Mkandarasi alikuwa ni M/S VALOSU COMPANY LIMITED, S.L.P. 1588, MWANZA.

v. Matengenezo ya kawaida katika barabara za makongoro na barabara za lami. Mkandarasi alikuwa ni M/S MILISA HOLDINGS LTD, S.L.P. 947, MUSOMA.

vi. Ujenzi wa mitaro na Kalvati katika barabara za Haile Selasie, Old Custom, Kawawa, Peace Palace - Field force Kwangwa na Kisurura. Mkandarasi alikuwa ni M/S VALOSU COMPANY LIMITED, S.L.P. 1588, MWANZA.

vii. Ujenzi wa barabara ya lami nyepesi - FFU - Cabin - Mutex Buhare km 0.33. Mkandarasi alikuwa ni M/S WHITE DOOR (T) LTD, S.L.P.1446, MUSOMA.

Matengenezo yote yaliyoainishwa hapo juu yalitumia jumla ya shilingi **1,297,543,306.35.**

Aidha idara ya ujenzi ilisimamia matengenezo ya barabara yaliyoanza kufanyika kwa kutumia fedha za mwaka 2016/2017. Matengenezo hayo ya barabara bado yanaendelea kama ifuatavyo;

i. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Bweri Madukatisa na Songambele, Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Rwamlimi, Matengenezo ya Muda maalumu katika barabara za Songambele, Bweri - Nyamitwebiri, Majengo - Rwamlimi na Songe - Kambarage - Iringo. Mkandarasi ni KITANGA CONTRACTORS LTD, S.L.P. 357 BUNDA.

ii. Matengenezo ya kawaida katika barabara Kwangwa, Mara Sekondari - Kiara, Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara za Kamunyonge, Bethsaida na Kigera, Matengenezo ya Muda maalumu katika barabara za Kwangwa na Kamunyonge na ujenzi wa mitaro katika barabara za Kwangwa na Bethsaida. Mkandarasi ni BEFEGE Investiment & Contructors Limited wa S.L.P.1544, MUSOMA.

iii. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Buhare na Nyamatare shule ya msingi - Kigera, Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Buhare,

Matengenezo ya Muda maalumu katika barabara za Kiara - Buhare na Nyamatare na ujenzi wa mitaro katika barabara ya Kiara – Buhare. Mkandarasi ni M/s Mhonwa Construction wa S.L.P.1009, SHINYANGA.

iv. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Mtakuja - Nyamiongo na Mwisenge - Majita (Nyamrasa), Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara za Mwisenge - Misango, Mtakuja - Makaburini na Makoko ziwani na ujenzi wa mitaro katika barabara Mwisenge - Misango, Mtakuja - Makaburini na Makoko ziwani. . Mkandarasi ni BEFEGE Investiment & Contractors Limited wa S.L.P.1544, MUSOMA.

v. Matengenezo ya muda maalumu katika barabara za [Sokoni (Shomoro), Kusaga, Mukendo, Shabani, Uhuru, Sokoni and Boma]. Mkandarasi ni Kalumo Technology Investment Limited wa S.L.P. 235 MUSOMA.

vi. Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara za Iringo na Old Custom Matengenezo ya muda maalumu katika barabara za Makoko na Maktaba na ujenzi wa mitaro katika barabara ya Old Custom. Mkandarasi ni DM & C Construction Company Limited wa S.L.P. 605, MUSOMA.

vii. Matengenezo ya kawaida katika barabara ya Nyasho ; Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara za Kitaji na Nyasho; Matengenezo ya Muda maalumu katika barabara za Nyasho Cabin; Welfare na ujenzi wa mitaro katika barabara ya Welfare. Mkandarasi ni Lunyalula Construction Company Limited wa S.L.P. 11041, MWANZA.

viii. Ujenzi wa daraja katika barabara ya Mshikamano- Rwamlimi na ujenzi wa Kalvati na mitaro katika barabara ya Nyasho Cabin. Mkandarasi ni Maicha Engineering Investment Co. Limited, S.L.P. 1410 MUSOMA.

ix. Matengenezo ya kawaida katika barabara ya Nyakato - Mshikamano shule ya Msingi ; Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Magamaga; Matengenezo ya Muda maalumu katika barabara ya Mshikamano na Nyakato Sanane. Mkandarasi ni MHONWA CONSTRUCTION CO. LTD, S.L.P. 1009 SHINYANGA.

x. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Makoko, St Anthony Makoko, Mwisenge Makaburini, Nyabisare, Mukendo, Maktaba, Kamunyonge, Kawawa, Haile Sellasie, Kitaji Bondeni na Iringo ; Kazi za mitaro katika barabara za Majita - Makaburini, Mwisenge Makaburini, Bukanga, CCM -

NMB (Polisi), Mwigobero, Mwisenge Misango na Iringo. Mkandarasi ni Winners Company LTD, S.L.P. 1102, MUSOMA.

xi. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Nyasho Majita, Nyamatare, Mukendo SDA Church, na Kusaga ; Kazi za mitaro katika barabara za Nyasho Cabin - Magereza , Nyasho - Magereza, Nyasho Majita & Nyamatare. Mkandarasi ni Makima General Traders, S.L.P. 8356, DAR ES SALAAM.

xii. Matengenezo ya kawaida katika barabara ya Majengo Mapya na Bweri Paroma, Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Nyakato sanane ; Kazi za mitaro katika barabara za Kwangwa - Kiara, Bweri Maduka Tisa, Buhare Bima na Kiara Gengeni. Mkandarasi ni Gem Engineers Co Ltd, S.L.P. 384, MUSOMA.

Hadi tarehe 30 Juni, 2017 kiasi cha shilingi **406,603,357.36** kilikuwa kimetumika kati ya shilingi **638,526,205.38** zilizokuwa zimekwishapokelewa.

Pia Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilianza kazi ya uboreshaji wa barabara kupitia programu ya uboreshaji miji (ULGSP) lengo likiwa ni kuboresha barabara zenye urefu wa **km 9.867** kwa gharama ya shilingi **9,930,059,618.54** na Mkandarasi ni M/S Nyanza Road Works. Aidha kazi ya kusimamia uboreshaji wa **km 9.867** utafanywa na Mhandisi mshauri ambaye ni Norplan Co. Ltd kwa gharama ya shilingi **883,000,000.00**.

17.0 Kitengo cha Nyuki

Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na;

i. Kikundi kipya cha community alive kimeanzishwa na kufanikiwa kufunga mkataba na mfuko wa misitu Tanzania (TFF) chini ya udhamini wa Halimashauri ya Manisipaa kuweza kupata ruzuku ya shilingi **20,000,000.00** kwa ajili ya kuambika mizinga **100** katika eneo la Bweri.
ii. Vikundi vliivyopo vimehamasishwa kuongeza idadi ya mizinga na kukarabati mizinga mibovo (mizinga **14** imekarabatiwa na kufanyiwa usafi).
iii. Kuteketeza na kuhamisha makundi ya nyuki yaliyo vamia makazi ya watu maeneo ya Free pack, Kariakoo, Airpot na Kituo cha afya cha Anglican Bweri.

Shughuli zote zilizotekelezwa ziligharimu shilingi **6,425,000.00.**

18.0 Kitengo cha Sheria na Usalama

Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na;

i. Kuendelea kusimamia kesi za madai **40** ambazo ziko katika mahakama mbalimbali (Mahakama Kuu ya Tanzania – Mwanza, Mahakama ya Wilaya – Musoma, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya – Musoma, Mahakama ya Hakimu Mkazi – Musoma na Tume ya Usuluhishi na uamuzi wa Migogoro ya kazi (CMA)).
ii. Kuendelea kutoa ushauri kwa lengo la kumaliza kesi kwa kuzingatia misingi ya haki na ushauri huo ulilenga kuzuia hasara zaidi zinazoweza kujitokeza upande wa Halmashauri.
iii. Kuondoa wafanyabiashara katika maeneo yasiyoruhusiwa maeneo ya Manota kata ya Mwigobero, Stendi ya zamani, Serengeti na Bustani ya Malkia.
iv. Kukamata mifugo iliyokuwa inazurura mjini na kutozwa faini ikiwa ni pamoja na kutoa onyo kwa wamiliki wa mifugo hiyo. Ng'ombe **180**, mbuzi **80** na kondoo **7** walikamatwa.
v. Kuandaa marekebisho ya sheria ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Shughuli zote ziligharimu shilingi **26,129,971.25**.

18.0 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Kitengo cha ukaguzi wa ndani kina jukumu la kufanya ukaguzi wa kawaida kwa muijbu wa sheria Na. 34 ya kanuni za fedha toleo la 2001 ikisomwa pamoja na kanuni Na. 14 ya sheria za fedha ya serikali za mitaa ya mwaka 2010 (LAFM).

Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na;

i. Kufanya ukaguzi wa kwa ajili ya kufanya tathimini kwa shughuli zilizofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 kwa kufanya ukaguzi wa nyaraka (Transaction Audit) na ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Lengo likiwa ni kulinganisha ufanisi wa Halmashauri na malengo ya serikali kwa madhumuni ya kuongeza umakini katika maeneo yasiyofanya vizuri, uwajibikaji na kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inafikiwa katika matumizi ya rasilimali za serikali.

ii. Kufuatilia ili kujiridhisha kama mfumo wa udhibiti wa ndani unafanya kazi na kufuatilia hoja za nyuma.

iii. Kuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani kwa kila robo mwaka .

Shughuli zote zilizoharimu shilingi **7,714,000.00**.

Mhe. Mwenyekiti,

Halmashauri katika kutekeleza shughuli mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilikabiliwa na changamoto zifuatazo;

Na	**Changamoto**	**Suluhisho**
1.	Kutotolewa kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na fedha za uendeshaji wa Halmashauri (OC).	Serikali kuu iombwe kutoa fedha kwa mujibu wa mpango kazi wa Halmashauri
2.	Ukosefu wa gari kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo	Kununua gari kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo
3.	Upungufu wa watumishi hususan katika idara za Afya, Elimu msingi na sekondari	Kufuatilia vibali vya ajira na kuajiri watumishi
4.	Mifugo inayozaga na kula miche ya miti iliyopandwa	Kudhibiti mifugo inayo zagaa mjini.
5.	Upungufu wa vitendea kazi	Kununua vitendea kazi
6.	Uhaba wa magari ya kusomba taka ngumu na maji taka	Ununuzi wa magari

19.0 Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti,

Kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha na kuomba Baraza lako lipitie na kujadili taarifa hii inayoonyesha shughuli zilizotekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Fidelica G. Myovella
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA,
MUSOMA